**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIMKARIBISHA MHE. MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) KUFUNGUA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA OFISI ZA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI DODOMA TAREHE 19 DISEMBA, 2023**

---

- **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;**
- **Mhe. Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Beatrice Jeremiah Nzobonaliba, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Katibu wa TUGHE Jiji la Dodoma;**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Bi. Zella Kiliat Lwemanyila, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Wanahabari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya na fursa ya kuweza kukutana hapa siku ya leo katika Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pili, ninakushukuru sana kwa utayari wako na kwa kukubali ombi letu la kuwa mgeni rasmi katika Mkutano huu. Tunafahamu kwamba, unayo majukumu mengi makubwa na muhimu katika nchi hii, lakini baada ya kukufahamisha kuwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameshindwa kufika kutokana na sababu ambazo hazikuweza kuzuilika, umeweza kutenga muda na kufika hapa ili kutufungulia mkutano huu na kupata fursa ya kukutana na wawakilishi wa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. **Tunasema asante sana kwa kuitikia mwaliko wetu.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Kwa niaba ya watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Tunaahidi kuendelea kukupa ushirikiano wa dhati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yako kama tulivyofanya wakati ukiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Nitumie fursa hii pia kumpongeza tena Mhe. Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gastorn kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Mhe. Jaji Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa aliyeteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Tunaahidi kukupatia ushirikiano wa kutosha wakati wa utekelezaji wa majukumu yako. Pia, tunakukaribisha kuwa mjumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo. **Hongereni sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Niwashukuru na kuwapongeza Wakuu wa Divisheni na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taaluma, maarifa, weledi na uzalendo. Aidha, naipongeza Sekretarieti na wote waliohusika kuandaa mkutano huu. Shukrani za dhati ziende kwa wageni waalikwa kwa kukubali mwaliko wetu. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito lakini kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu, mmeacha shughuli zenu ili muweze kujumuika nasi hapa siku ya leo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa chini ya Ibara ya 59 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kupewa jukumu la kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria ndani na nje ya nchi. Ofisi inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 pamoja na sheria mbalimbali za kazi, kama vile, Agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2003, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 na Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105.

Kwa mujibu wa sheria hizo, pamoja na mambo mengine, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Taasisi nyingine za Umma zinapaswa kuwashirikisha wafanyakazi wao katika masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya watumishi, uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti na kujadili hoja mbalimbali zinazotokana na utekelezaji wa mpango na bajeti ili kuzishauri menejimenti ipasavyo. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 13.1 (c) ya Mkataba wa kuunda Baraza la Wafanyakazi kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na TUGHE wa mwaka 2020, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapaswa kufanya Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi si chini ya mara mbili kwa mwaka. Mkutano wa mwisho kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulifanyika jijini Dodoma tarehe 18 Aprili, 2023 kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya

Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mkutano huu ni mkutano wa kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ajenda kuu za Mkutano huu ni kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 na taarifa ya hesabu za mwaka 2022/2023. Kwa mantiki hiyo, ajenda za Mkutano huu zinalenga kupima mafanikio ya utekelezaji wa mpango na bajeti na mizania ya mahesabu ya mwaka 2022/2023. Hivyo, baada ya Mkutano huu kufunguliwa rasmi, wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watapata fursa ya kupokea na kujadili hoja mbalimbali zitakazoibuliwa katika taarifa hizo na kisha kutoa mapendekezo mbalimbali ambayo yatawasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Baada ya maelezo hayo, ninapenda pia kuwajulisha kuwa, katika Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulioishia mwezi Juni, 2023, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutekeleza Mpango Kazi wake kama ifuatavyo:

**(a) Ajira**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Mahitaji ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni **477** katika Mikoa yote **26**. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Watumishi **50** waliajiriwa na Ofisi

ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo kati ya hao, Watumishi **48** ni Mawakili wa Serikali na Maafisa TEHAMA **2**. Jumla ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mpaka sasa ni **192** ambapo kati ya hao, **177** wapo kwenye *payroll* ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, watumishi **111** ambayo ni sawa na **37%** ni Mawakili wa Serikali, watumishi **66** ni kada nyingine na watumishi **15** wameazimwa kutoka taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:

- watumishi **5** wameazimwa kutoka Jeshi la Polisi Tanzania;
- watumishi **3** wameazimwa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
- mtumishi **1** ameazimwa kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;
- watumishi **2** wameazimwa kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania;
- mtumishi **1** ameazimwa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje;
- mtumishi **1** ameazimwa kutoka Ofisi ya Rais – Ikulu;
- mtumishi **1** ameazimwa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria; na
- mtumishi **1** ameazimwa kutoka Mahakama ya Tanzania.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali bado ina upungufu wa watumishi **285** ambayo ni sawa na **63%.** Hivyo, jitihada za kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali na Watumishi wa kada nyingine zinaendelea ikiwa ni pamoja na kuomba kuongezewa Watumishi kwa njia ya uhamisho wa ndani ya Serikali na kupewa kibali cha ajira mpya kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kupitia Wizara ya Katiba na Sheria. Aidha, mwaka 2022/2023, Watumishi **11** walipandishwa vyeo, Mtumishi **1** alifanyiwa *re-categorization* na Watumishi **39** walithibitishwa kazini.

**(b) Mafunzo**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Mwaka 2022/2023, Watumishi **13** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali kama vile Uandishi wa Nyaraka za Kisheria, Usimamizi wa Mikataba, TEHAMA, Uhasibu, Manunuzi, Uchumi na Takwimu. Pia, Watumishi **29** walihudhuria Mafunzo, Warsha na Semina mbalimbali ndani na nje ya nchi na Watumishi **50** walioajiriwa walipatiwa Mafunzo Elekezi (induction course).

Aidha, Mawakili wa Serikali **38** walioajiriwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 2022/2023 walipelekwa katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kupata mafunzo ya namna ya kuendesha mashauri ya jinai kwa lengo la kuwajengea uwezo wa Kitaalamu na Kitaaluma. Mawakili wa Serikali **10** kati ya **38** waliopelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wamesharejeshwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanaendelea kutekeleza majukumu yao katika Divisheni ya Uandishi wa Sheria.

**(c) Vifaa vya TEHAMA**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kununua na kupatiwa vifaa vya TEHAMA kutoka kwa wadau mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) moja **(1)**, Printa (Hp Laserjet & Pro MFP) mbili **(2)** na Kompyuta za mezani (Hp Elite) nne **(4)** kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT);

(b) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) nne **(4)** kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);

(c) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) tano **(5)**, Kompyuta za mezani (Hp 200 G4 – ALL–IN-ONE) tano **(5)** na Printa (Hp Color Laserjet Pro M454dw) moja **(1)** kutoka Kampuni ya Kagera *Sugar* (Superdoll);

(d) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) tatu **(3)**, Kompyuta za mezani (Hp 200 G4) kumi **(10)** na Printa (Hp Laserjet Pro M454dw) mbili **(2)** kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

(e) Kompyuta Mpakato (Hewlet Packard (HP) kumi **(10)** kutoka Kampuni ya *Williamson Diamond Limited*;

(f) Vishikwambi (Tablets – ZTE BLADE X10s) Hamsini **(50)** kutoka Wizara ya Elimu kupitia *National Bureau of Statistics* (NBS);

(g) Kompyuta Mpakato Sitini **(60)** (Hp envy) kati ya Mia Hamsini **(150)** ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia ahadi aliyoitoa siku ya Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali;

(h) Kompyuta za mezani (Desktop) nne **(4)**, Kompyuta Mpakato aina ya *Macbook* nne **(4)**, Kompyuta Mpakato aina ya *HP Spectre x 360* ishirini na sita **(26)**, *Multi Sites Video Conferencing* moja **(1)**; *Point to Point Video*

*Conferencing* moja **(1)**, *Scanner* tatu **(3)**, *Heavy Duty Photocopy Machine* moja **(1)** na *White Boards* mbili **(2)** kupitia ufadhili wa Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania *(Building Sustainable Anti- Corruption Action Tanzania* (BSAAT);

(i) Kompyuta za mezani (Desktop) aina ya *Dell* zipatazo ishirini na sita **(26)**, Kompyuta Mpakato aina ya *Dell Latitude* zipatazo ishirini na sita **(26)** na Printa aina ya HP Lasejet Pro MFP 428 FDW ishirini na sita **(26)** kutoka Mahakama ya Tanzania katika Utekelezaji wa Mapango Mkakati wa Mahakama wa Maboresho hususan katika eneo la Ushirikishwaji wa Wadau.

(j) Kompyuta Mpakato aina ya *Dell Latitude* zipatazo kumi **(10)** pamoja na Scanner Jet Pro moja **(1)** kutoka Giz Digitalization of Law; na

(k) Kompyuta Mpakato kumi **(10)** aina ya HP Spectre X 360 kutoka kwa wadau wetu wengine.

Jumla ya vifaa hivyo ni Kompyuta Mpakato **159**, Vishikwambi **50**, Kompyuta za Mezani **49**, Printa **31**, *Heavy Duty Photocopy Machine* moja **(1)**, *Scanner* **4**, *Multi Sites Video Conferencing* **1**, *Point to Point Video Conferencing* **1** na *White Boards* **2**. Mpaka sasa **85%** ya watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wameshapatiwa vifaa hivyo vya TEHAMA.

Kwa niaba ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nitumie fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali na wadau wote waliotajwa hapo juu kwa kutupatia vitendea kazi hivyo ambavyo vinasaidia sana kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**(d) *Office of the Attorney General Management of Information System* (OAG–MIS)**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Mnamo tarehe 29 Septemba, 2022 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua mfumo wa OAG–MIS. Pamoja na mambo mengine, mfumo huo una dirisha la kupakia sheria, Daftari la Usajili wa Mawakili wa Serikali, Dawati la Msaada (*help desk)* na Simu ya Huduma kwa umma *(Toll Free Number)*.

Hadi kufikia tarehe 14 Desemba, 2023, jumla ya Mawakili wa Serikali **3,359** walikuwa wamesajiliwa na kuhuisha taarifa zao katika mfumo wa OAG-MIS ambapo kati yao, **1,667** pia ni Wanachama wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) na **307** wakiwa ni Wanasheria wa Serikali ambao wanatekeleza majukumu yao chini ya TAMISEMI.

Mfumo huu wa OAG-MIS umesaidia sana kuongeza kasi ya utendaji kazi kwa Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wadau na Umma kwa ujumla. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na mpango wa kuweka

mifumo madhubuti ya kielektroniki na kuunganisha mfumo wa OAG-MIS na mifumo mingine kama vile Mfumo wa Kesi wa Mahakama ya Tanzania (e-cms), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

**(e) Programu ya Elimu kwa Umma kuhusu Sheria na Haki**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa Watanzania **95** katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria. Programu mbili **(2)** za kwenye Televisheni zinazohusu huduma za utoaji wa uelewa wa sheria ziliandaliwa na kurushwa wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mawakili wa Serikali uliofanyika mwaka 2022. Aidha, Kikoa (website) cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilihuishwa na makala, shajara na kalenda ziliandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali ili kujenga uelewa wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**(f) Government Legal Institutions Integrated Centers – GLIICs**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Majengo ya Vituo Jumuishi katika mikoa ya Mwanza na Arusha pamoja na Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jijini Dodoma. Vituo Jumuishi vinajumuisha Taasisi za

Serikali zinazotoa Huduma za Kisheria ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wadau wake.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2023, gharama za mradi wa ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi katika mkoa wa Mwanza zilikuwa zimefikia kiasi cha Shilingi **1,153,335,586.80** sawa na **36%** ya Bajeti ya mradi ambayo ni Shilingi **3,180,815,233.81** ambapo Mkandarasi alikuwa amepokea kiasi cha Shilingi **1,097,797,474.30** na Mshauri Mwelekezi alikuwa amepokea kiasi cha Shilingi **55,538,112.50**. Mpaka kufikia tarehe 11 Novemba, 2023, ujenzi ulikuwa umefikia **80%.**

Aidha, hadi kufikia mwezi Juni, 2023, gharama za mradi wa ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi katika mkoa wa Arusha zilikuwa zimefikia kiasi cha Shilingi **627,292,608.94** sawa na **17%** ya Bajeti ya mradi ya Shilingi **3,714,194,595.75** ambapo Mkandarasi alikuwa amepokea kiasi cha Shilingi **526,853,536.94** na Mshauri Mwelekezi alikuwa amepokea kiasi cha Shilingi **100,439,072**. Kwa mradi huu, hadi kufikia tarehe 11 Novemba, 2023, ujenzi ulikuwa umefikia **12%.** Changamoto kubwa inayoukabili mradi huu ni ucheleweshaji wa fedha kwa mkandarasi.

Ujenzi wa Vituo Jumuishi, kama ulivyoidhinishwa na Serikali unalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za kisheria zitolewazo na taasisi husika na kuwapunguzia gharama wadau na wananchi, kuongeza kasi na wigo wa upatikanaji wa huduma hizo kwa wakati na kupunguza gharama za uendeshaji wa Ofisi kwa kuepukana na gharama za kila taasisi kujenga au kupanga pango lake.

Hadi kufikia tarehe 11 Novemba, 2023, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaoendelea katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma lenye uwezo wa kutumiwa na watumishi zaidi ya 500 kwa wakati mmoja ulikuwa umefikia **63%**.

**(g) Mradi wa Kujenga Uwezo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (Building Sustainable Anti – Corruption Action In Tanzania – BSAAT)**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Kuzijengea Uwezo Taasisi za Umma zinazohusika na Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Building Sustainable Anti-corruption Action in Tanzania – BSAAT). Hadi kufikia mwezi Juni, 2023, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa imepokea na kutumia Shilingi **474,929,227.30** sawa na **95%** ya Bajeti ya Shilingi **500,000,000.00** na kufanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kujenga Mfumo wa Usimamizi wa taarifa (Data Management System) unaoshughulikia Mikataba, Malalamiko na Mashauri ili kuwezesha tathmini na ufuatiliaji kwa urahisi pamoja na kuweka kanzidata za nyaraka hizo. Ujenzi wa mfumo huo umefanyika chini ya e-GA ambapo sasa unafanyiwa majaribio kabla ya kuukabidhi kwa OMMS;

(ii) Kupitia na kuchambua mikataba mikubwa yenye viashiria vya rushwa kubwa;

(iii) Kupitia na kuchambua malalamiko na mashauri yenye viashiria vya rushwa kubwa;

(iv) Kufanya ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kama ilivyoelezwa hapo juu ambavyo ni Kompyuta za mezani (Desktop) nne **(4)**, Kompyuta Mpakato aina ya *Macbook* nne **(4)**, Kompyuta Mpakato aina ya *HP Spectre x 360* ishirini na sita **(26)**, *Multi Sites Video Conferencing* moja **(1)**; *Point to Point Video Conferencing* moja **(1)**, *Scanner* tatu **(3)**, *Heavy Duty Photocopy Machine* moja **(1)** na *White Boards* mbili **(2);**

(v) Kuwezesha Mawakili wa Serikali **41** kupatiwa mafunzo kuhusu Miongozo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzia tarehe 18–21 Aprili, 2023 jijini Dodoma. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuongeza uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika maeneo ya Utungaji wa Sheria, Upekuzi wa Mikataba na Utoaji Huduma za Ushauri wa Kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kumwezesha Wakili wa Serikali mmoja **(1)** kushiriki mafunzo kwa vitendo (attachment) katika Kituo cha Usuluhishi cha Kimataifa cha *Asian International Arbitration Centre* (AIAC)) huko Kuala Lumper, Malaysia kuanzia tarehe 18 Juni, 2023 hadi tarehe 3 Julai, 2023 ili kumpatia ujuzi na uzoefu katika eneo la Usuluhishi wa Kimataifa; na

(vii) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa BSAAT.

**(h) Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (Tanzania Public Bar Association -TPBA)**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Natoa pongezi za dhati kwa Uongozi wa mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (Tanzania Public Bar Association – TPBA) chini ya Bw. Michael Luena na Bi. Sia Beatrice Mrema, Rais na Katibu wa Chama mtawalia, pamoja na safu yao ya uongozi kwa mambo kadhaa waliyotekeleza tangu wateuliwe na kuwekwa kazini tarehe 30 September, 2022. Aidha, natoa shukrani kwa Wizara, Taasisi za kisheria ikiwemo TLS na mawakili wote kwa kuwapatia ushirikiano uliowawesha kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa.

Katika Mkutano wa Pili wa Chama utakaoitishwa na kufanyika kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa fedha 2023/24, ninayo matumaini makubwa kuwa kwa msingi uliokwishawekwa na Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Uongozi wa Muda, Mawakili wa Serikali na washiriki watapata fursa zaidi ya kutekeleza majukumu ya Chama chao pamoja na kushiriki katika Mada mbalimbali zitakazowasilishwa. Hivyo, nawaomba Mawakili wa Serikali mliopo hapa muwasihi wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali wajiandae kuhudhuria bila kukosa.

(i) **Majukumu ya Divisheni**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Kwa ujumla, mwaka 2022/2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza majukumu mbalimbali kupitia Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria, Divisheni ya Mikataba na Makubaliano na Divisheni ya Uandishi wa Sheria ikiwemo:

(i) Kuendesha, kusimamia na kushiriki katika majadiliano na mashauri ya madai na jinai mahakamani;

(ii) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Kushiriki katika vikao vya Kikanda na Kimataifa ambavyo Serikali ina maslahi;

(iv) Kuandaa miswada ya Sheria **17**, kutafsiri sheria **319**, kufanya zoezi la urekebu wa sheria **741** na sheria ndogo **829**;

(v) Kufanya upekuzi wa mikataba **1,777** na Randama za Maelewano **466;** na

(vi) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambapo idadi ya ushauri huo ni **1,252**. Maombi ya ushauri wa kisheria yaliyowasilishwa kutoka TAMISEMI mwaka wa fedha 2020/21 yalikuwa **65**, mwaka 2021/22

TAMISEMI iliwasilisha maombi **68** na mwaka 2022/2023, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea maombi **281** kutoka TAMISEMI.

Maboresho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu yaliyofanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018 yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji hususan katika utoaji wa ushauri wa kisheria, upekuzi wa mikataba, uandishi wa sheria ndogo na uendeshaji na usimamizi wa mashauri kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**(j) Kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Itakumbukwa kuwa, mnamo tarehe 31 Oktoba, 2023, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu, pamoja na mambo mengine, lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria (Na. 11) ya 2023 (The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Act. No. 11 of 2023) ambayo, pamoja na mambo mengine, ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 na kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia vifungu vya 3, 7A, 7B, 8, 8A, 8B, 10, 10A, 12, 12A na Nyongeza ya Sehemu ya VIII kuhusiana na masuala ya fedha.

Lengo mahsusi la mabadiliko hayo ni kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kukidhi mahitaji ya nchi yetu baada ya kuanza kutekeleza maboresho makubwa kwenye eneo la Utawala wa Sheria, misingi ya Utawala Bora na mifumo ya utoaji Haki. Ni matarajio yangu kuwa tutaongeza kasi ya kutafiti, kuandika, kutafsiri na kurekebu sheria pamoja na kuhakikisha sheria ndogo zinazotungwa na mamlaka zilizokasimiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya hivyo, hazikinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria Mama. Wizara ya Katiba na Sheria na Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zimeombwa kusaidia kuziwezesha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Fedha kukamilisha taratibu zitakazoiwezesha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Serikali kutengewa Bajeti yake hivyo kuzipatia wepesi Divisheni nyingine za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Changamoto kubwa zinazoikabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni upungufu wa bajeti ya kuendesha shughuli za Ofisi, upungufu wa watumishi, ufinyu wa nafasi za Ofisi na uhaba wa magari ambapo Ofisi ina jumla ya magari **16** wakati mahitaji ni magari **45**. Kati ya magari hayo, magari **13** yapo katika hali nzuri na yanatumika na magari **3** ni mabovu na yanahitaji matengenezo. Pia, Ofisi ina bajaji mbili ambazo zote zinatumika na mabasi mawili ambayo yanatumiwa na watumishi.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inaendelea kuwasiliana na Mamlaka pamoja Wizara na Taasisi zetu katika kupata ufumbuzi wa changamoto hizo. Hata hivyo, pamoja na changamoto hizo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza mpango kazi wake na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha wajumbe wa Baraza waliopo hapa ambao ni wawakilishi wa watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzingatia masuala yafuatayo wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku:

**(a) Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaongozwa na Dira na Dhima zifuatazo:

***Dira: Kuwa Taasisi yenye ufanisi, kitaaluma na kuaminika katika kutoa huduma bora za kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.***

***Dhima: Kutoa Huduma za Kisheria zenye ubora kwa njia ya kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa.***

Ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira na Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na misingi mikuu minne ambayo ni

**utaalamu/weledi, ubunifu, uadilifu na uwazi.** Maafisa waandamizi tulio hapa, ni jukumu letu kuhakikisha Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekelezwa ili kufikia Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo, kama viongozi, ni vema tuzingatie maneno yafuatayo wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku:

> ***"Leadership is the capacity to translate vision into reality. If you fulfill the vision of the employees, the employees will fulfill your vision".***

Nawasihi viongozi wenzangu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tujitahidi kuwatimizia mahitaji mbalimbali watumishi walio chini yetu yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi ili nao watoe huduma za kisheria zenye ubora na hatimaye tuweze kutimiza malengo ya Dira yetu.

**(b) Mkataba wa Huduma kwa Wateja**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa mwaka 2022 unawataka watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutumia lugha nzuri yenye staha wakati wa kuhudumia wateja wetu. Tunapotoa huduma za kisheria kwa wadau mbalimbali kwa niaba ya Serikali, tunapaswa kuhakikisha wateja wetu wanapata huduma hiyo kwa wakati ndani ya muda ulioanishwa katika Mkataba huo.

**(c) Tathmini ya Utendaji Kazi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Hivi karibuni nimebaini uwepo wa dosari za kimaandishi na kimaudhui katika kazi zinazotoka nje ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo, natumia fursa hii kuwataka Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kuhakikisha mnapitia na kujiridhisha na kazi zilizofanywa na maafisa ambao wapo chini yenu kabla kazi husika haijatoka nje ya Ofisi. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kujenga uaminifu kuhusu ubora wa kazi zetu. Aidha, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu unapaswa kuhakikisha watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanatumia mfumo mpya ujulikanao kama Mfumo wa kutathmini utendaji kazi wa watumishi katika sekta ya umma (Public Employees Perfomance Management of Information System-PEPMIS) kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Nachukua fursa hii pia kuipongeza Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kusimamia vyema masuala ya Utendaji, Utawala na Rasilimali watu na kuiwezesha Ofisi yetu kufanyiwa tathmini katika zoezi lililofanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kushika nafasi ya pili katika Kundi la Idara za Serikali zinazojitegemea. Hongera sana Mhe. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Menejimenti na watumishi

wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa matokeo hayo. Naamini tathmini ijayo tutashika nafasi ya Kwanza. **INAWEZEKANA.**

**(d) Nidhamu kwa Watumishi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kunakuwa na nidhani ya kazi, maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya Wafanyakazi na Menejimenti ili kuleta tija na ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kufahamu kwamba ni wajibu wetu kuheshimiana bila kujali tofauti zetu za kada na wadhifa tulionao. Hatua za kinidhamu zichukuliwe mara moja kwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watakaobainika kuharibu taswira ya Ofisi yetu kwa kwa kujihusisha na vitendo vilivyo kinyume na maadili ya utumishi wa umma kama vile uzembe, rushwa na udanganyifu. Katika hili, Kanuni zetu za Maadili dhidi ya mawakili wanaokiuka maadili katika utekelezaji wa majukumu yetu - "The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Provision of Legal Opinion by State Attorneys and Law Officers in Public Service) Guidelines, G.N 32/2023 zilizochapishwa tarehe 20 Januari, 2023 zitatumika ipasavyo.

### (e) Maslahi ya Watumishi

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kufanya maboresho ya maslahi ya Watumishi kila mwaka. Nitumie fursa hii kuwafahamisha kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 8(3) (d) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 8A(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, tarehe 20 Septemba, 2023 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa Waraka wa idhini ya malipo ya posho na stahili za Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanaotekeleza majukumu yao katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Umma, Wakala wa Serikali na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kupitia Waraka huo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024, Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria hao wanapaswa kulipwa posho na ada mbalimbali ikiwemo posho ya vazi maalum kwa Mawakili (Court Attire Allowance), posho ya usaidizi wa pango (Rent Housing allowance), ada ya Chama cha Mawakili wa Tanzania Bara (TLS), ada ya Kamishna wa Viapo wa Mahakama Kuu kwa Mawakili walioapishwa kutunza tange, ada ya Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na posho ya simu kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika waraka. Hata hivyo na kwa kuzingatia mazingira ya kipekee, kuanzia mwaka 2022/2023, watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walianza kulipwa posho ya usaidizi wa pango la nyumba.

Kuhusu maombi ya muundo wa Mishahara ya Watumishi wote katika Ofisi Kuu za Kisheria ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, mawasiliano yanaendelea kufanyika na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshawasilisha Wizara ya Fedha maombi ya kuongezewa ukomo wa Bajeti ili iweze kukamilisha majukumu yake ambayo yameshaanza kutekelezwa lakini yanashindwa kukamilika kutokana na upungufu wa bajeti ikiwemo gharama za Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mawakili wote wa Serikali na ujenzi wa Vituo Jumuishi unaoendelea.

**(f) Mafunzo**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanatambua kuwa, miongoni mwa masuala ambayo nimekuwa nikitoa msisitizo mara kwa mara ni kuwahimiza kujiendeleza. Kwa kuzingatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na mbinu za kisasa za utendaji kazi, napenda kutoa rai kwenu nyote kuwa kila mmoja wenu anapaswa iwe kwa kujigharamia au kugharamiwa na Serikali ahakikishe anapata mafunzo ya muda mfupi au hata ya mrefu kwa madhumuni ya kwenda na wakati. Mimi binafsi ni mfano wa watumishi wa umma niliyejiendeleza kwa kusoma baadhi ya programu zangu nikiwa kazini ikiwemo Shahada ya Uzamivu niliyoanza mwaka 2006 na kuhitimu mwaka 2011.

Nazielekeza Menejimenti za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na mamlaka nyingine Serikalini kuweka vigezo mahsusi ambavyo tutavitumia kuwaombea vyeo vya msereleko Mawakili wa Serikali watakaovitelekeza kwa ufanisi pamoja na wasimamizi wao. Mfano wa vigezo hivyo ni: kila Wakili wa Serikali kuendesha mashauri ya aina mbalimbali kwa idadi itakayokubalika, kufanya tafiti katika maeneo yenye matokeo makubwa na kushiriki kikamilifu katika majukumu yanayopimika atakayopangiwa.

Katika zama hizi, ujuzi na ubunifu ndizo nyenzo kubwa za kukabiliana na changamoto hususan katika sekta ya sheria. Ubunifu katika kutekeleza majukumu mbalimbali ni jambo muhimu sana. Ubunifu unaweza kupatikana kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujisomea na kujifunza. Pamoja na jitihada binafsi za kujiendeleza, napenda kuendelea kuwahimiza Maafisa waandamizi kuwajengea uwezo maafisa walio chini yao ili kuwapatia ujuzi na uelewa wa majukumu mbalimabli kwa vitendo ikiwa ni njia mojawapo ya mikakati kabambe na mahsusi ya kurithisha majukumu.

**(g) Michezo kwa Watumishi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamekuwa wakishiriki katika mabonanza na michezo ya SHIMIWI kila mwaka kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa lengo la kujenga na kuimarisha afya zao, umoja, uhusiano na ushirikiano baina ya wafanyakazi kutoka taasisi mbalimbali za umma. Kipekee, nawapongeza

washiriki wetu katika michezo ya SHIMIWI ya mwaka huu kwa kulinganisha na mwaka jana kwani kwa mwaka huu, tuliibuka washindi wa pili katika mchezo wa Karata kwa wanaume, pia, tuliibuka washidi wa tatu katika mchezo wa mpira wa miguu kwa wanaume na kupewa makombe pamoja na medali. Naomba tuongeze ushiriki katika michezo na kupata vikombe vingi zaidi katika mashindano yanayokuja kwa kuzingatia pia kuwa michezo ni afya ambayo itaboresha ufanisi katika maeneo yetu ya kazi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Katika Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watapokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na taarifa ya hesabu za mwaka 2022/2023 za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naomba tutumie maazimio ya Mkutano huu kuboresha mpango kazi na bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata wa 2024/25 huku tukitambua kuwa Ofisi yetu itakuwa na majukumu mahsusi ya kutekeleza kwenye Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai, Chaguzi zinazokuja mwaka 2024 na 2025, kutoa Chapisho la Urekebu wa Sheria la mwaka 2023 mnamo mwaka 2024, Kutunga na kutafsiri sheria zote kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kushughulikia kwa ufanisi majadiliano na usikilizwaji wa mashauri yaliyo katika Mahakama za ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima naomba sasa nikukaribishe ili utoe Hotuba yako na kisha utufungulie rasmi Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Niwatakie heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka mpya wa 2024.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI KARIBU SANA**